**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

# CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA (CBE)

College of Business Education

## KOZI MAALUMU KWA WAFANYABIASHARA WADOGO NA WA KATI

Kampasi: Dar es Salaam · Dodoma · Mwanza · Mbeya

Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)kinatoa kozi maalumu za muda mfupi zilizoandaliwa kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo na wa kati nchini Tanzania. Kozi hizi huchanganya nadharia na mazoezi ya vitendo yanayoendana na mazingira halisi ya biashara, na hutolewa na wakufunzi wenye uzoefu wa kitaaluma na kibiashara.

**Muda wa kozi:** Kila kozi ina muda wa siku 3.

- Namna ya kujifunza: ana kwa ana katika kampasi za CBE, mahali pa mfanyabiashara, au kwa njia ya mtandao.
- Vyeti: kila mshiriki atakayemaliza kozi atapata cheti cha CBE.
- Gharama: gharama zimeoneshwa kwa kila mshiriki kwa Shilingi za Tanzania (TZS) na zinajumuisha ufundishaji, vifaa vya mafunzo na cheti. Punguzo hutolewa kwa vikundi na taasisi.
- Mafunzo maalum: kozi yoyote inaweza kuandaliwa mahususi kwa kikundi au taasisi kwa ratiba na mahitaji yatakayokubaliwa.

**Usajili na mawasiliano:** Kurugenzi ya Ushauri, Utafiti na Machapisho, Chuo cha Elimu ya Biashara, S.L.P. 1968, Dar es Salaam, Tanzania.

Simu: 0755 488 381 · Barua pepe: rector@cbe.ac.tz · Tovuti: www.cbe.ac.tz

| Na | Jina la Kozi | Malengo ya Kozi na Stadi Zitakazopatikana | Walengwa | Gharama (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Uandaaji wa Mpango wa Biashara** *(Business Plan Development)* | Kozi hii inalenga kumwezesha mshiriki kuanzisha na kukuza biashara kwa msingi wa mpango thabiti.<br>**Malengo na umahiri:**<br>• Kuelewa dhana ya ujasiriamali na mazingira ya biashara Tanzania.<br>• Kutambua na kuchambua fursa za biashara (market gap analysis).<br>• Kuandaa mpango kamili wa biashara (executive summary, operations, marketing, finance).<br>• Kuandaa makadirio ya kifedha (cash flow, profit & loss).<br>• Kupima hatari na mikakati ya kuzipunguza (risk management).<br>• Kuandaa pitch ya kuvutia wawekezaji. | • Wajasiriamali wanaoanza<br>• Wamiliki wa biashara ndogo<br>• Wahitimu wanaotaka kujiajiri | **150,000** |
| 2 | **Masoko ya Kidigitali na Biashara Mtandaoni** *(Digital Marketing & E-Commerce)* | Kozi inalenga kuongeza mauzo kupitia mifumo ya kidigitali.<br>**Malengo na umahiri:**<br>• Kutumia majukwaa ya mitandao (Facebook, Instagram, TikTok, WhatsApp Business).<br>• Kuandaa maudhui ya kibiashara (content creation & branding).<br>• Kuendesha kampeni za matangazo (paid ads).<br>• Kuuza bidhaa mtandaoni (online selling strategies).<br>• Kupima matokeo ya matangazo (analytics). | • Wajasiriamali<br>• Wafanyabiashara wadogo<br>• Vijana wa biashara mtandaoni | **150,000** |

| Na | Jina la Kozi | Malengo ya Kozi na Stadi Zitakazopatikana | Walengwa | Gharama (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 3 | **Usimamizi wa Fedha na Uhasibu kwa Biashara Ndogo**<br>*(Financial Management & Accounting for Small Business)* | Kozi inalenga kuongeza ufanisi wa matumizi ya fedha.<br>**Malengo na umahiri:**<br>• Kutunza kumbukumbu za fedha (record keeping).<br>• Kuandaa bajeti na kudhibiti matumizi.<br>• Kuelewa gharama, mapato na faida.<br>• Kutenganisha fedha binafsi na za biashara.<br>• Kutumia zana rahisi za uhasibu (Excel, apps). | • Wamiliki wa biashara<br>• Mameneja wa biashara ndogo | **150,000** |
| 4 | **Huduma Bora kwa Wateja na Ujenzi wa Uaminifu**<br>*(Customer Care & Retention)* | Kozi inalenga kuongeza uaminifu na kurudi kwa wateja.<br>**Malengo na umahiri:**<br>• Kuelewa mahitaji ya wateja.<br>• Mbinu za kuhudumia wateja kitaalamu.<br>• Kushughulikia malalamiko na migogoro.<br>• Kujenga uhusiano wa muda mrefu (customer loyalty).<br>• Kutumia feedback kuboresha huduma. | • Wahudumu<br>• Wafanyabiashara<br>• Wajasiriamali | **150,000** |
| 5 | **Ubunifu, Uongezaji Thamani na Ufungashaji wa Bidhaa**<br>*(Product Innovation, Value Addition & Packaging)* | Kozi inalenga kuongeza ushindani wa bidhaa sokoni.<br>**Malengo na umahiri:**<br>• Ubunifu wa bidhaa mpya (product innovation).<br>• Uongezaji thamani (value addition).<br>• Ufungashaji bora na unaovutia (packaging & labeling).<br>• Viwango vya ubora (quality standards – TBS, TMDA).<br>• Branding ya bidhaa. | • Wazalishaji wadogo<br>• Vikundi vya wanawake na vijana | **150,000** |
| 6 | **Ujasiriamali kwa Vijana na Wanawake**<br>*(Entrepreneurship for Youth & Women)* | Kozi inalenga kukuza uwezo wa kiuchumi kwa makundi maalum.<br>**Malengo na umahiri:**<br>• Kujenga mtazamo wa kijasiriamali (entrepreneurial mindset).<br>• Kutambua fursa ndogo zenye faida.<br>• Kuanzisha na kusimamia biashara ndogo.<br>• Kujenga nidhamu ya fedha.<br>• Kujifunza kutoka kwa mifano halisi ya mafanikio. | • Vijana<br>• Wanawake<br>• Vikundi vya kijamii | **150,000** |
| 7 | **Upatikanaji wa Mitaji, Mikopo na Uwekezaji**<br>*(Access to Capital, Credit & Investment)* | Kozi inalenga kuwawezesha washiriki kupata na kusimamia fedha.<br>**Malengo na umahiri:**<br>• Kutambua vyanzo vya mitaji (benki, SACCOS, fintech).<br>• Kuandaa nyaraka za mkopo.<br>• Kuelewa masharti ya mikopo.<br>• Kusimamia deni na marejesho.<br>• Kuvutia wawekezaji. | • Wajasiriamali<br>• Vikundi vya SACCOS | **150,000** |

| Na | Jina la Kozi | Malengo ya Kozi na Stadi Zitakazopatikana | Walengwa | Gharama (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 8 | **Sheria, Kodi na Taratibu za Biashara Tanzania**<br>*(Business Law, Taxation & Procedures in Tanzania)* | Kozi inalenga uendeshaji sahihi wa biashara kwa mujibu wa sheria.<br>**Malengo na umahiri:**<br>• Usajili wa biashara (BRELA).<br>• Leseni na vibali.<br>• Mfumo wa kodi (TRA).<br>• Haki na wajibu wa mfanyabiashara.<br>• Kuepuka adhabu na migogoro ya kisheria. | • Wajasiriamali<br>• Wamiliki wa biashara | **150,000** |
| 9 | **Matumizi ya Teknolojia na Mifumo ya Kidigitali katika Biashara**<br>*(Technology & Digital Systems in Business)* | Kozi inalenga kuongeza ufanisi kwa kutumia TEHAMA.<br>**Malengo na umahiri:**<br>• Kutumia mifumo ya POS na programu-tumizi za biashara.<br>• Malipo ya kidigitali (M-Pesa, Tigo Pesa, Airtel Money).<br>• Usimamizi wa taarifa za biashara.<br>• Usalama wa taarifa (cybersecurity basics). | • Wajasiriamali<br>• Wafanyabiashara wadogo | **150,000** |
| 10 | **Usimamizi wa Ugavi, Ununuzi na Stoo**<br>*(Supply Chain Management)* | Kozi inalenga kuongeza ufanisi wa upatikanaji wa bidhaa.<br>**Malengo na umahiri:**<br>• Usimamizi wa stoo (inventory control).<br>• Uchaguzi wa wasambazaji bora.<br>• Kupunguza gharama za manunuzi.<br>• Usafirishaji na usambazaji (logistics).<br>• Kuepuka upotevu na wizi wa bidhaa. | • Wafanyabiashara<br>• Wamiliki wa maduka<br>• Wasimamizi wa ugavi | **150,000** |
| 11 | **Usimamizi wa Wafanyakazi wa Biashara**<br>*(Employee Management for Small Business)* | Kozi hii inalenga kumwezesha mshiriki kusimamia wafanyakazi kwa ufanisi ili kuongeza tija na ukuaji wa biashara.<br>**Malengo na umahiri:**<br>• Kuelewa dhana ya uongozi na usimamizi wa rasilimali watu katika biashara ndogo.<br>• Kuajiri, kupanga kazi na kugawa majukumu kwa ufanisi.<br>• Kuweka mfumo wa tathmini ya utendaji kazi (performance appraisal).<br>• Kujenga motisha na nidhamu kazini.<br>• Kutatua migogoro ya kikazi.<br>• Kuzingatia sheria za kazi na ajira Tanzania. | • Wamiliki wa biashara ndogo<br>• Mameneja<br>• Wasimamizi wa biashara | **150,000** |
| 12 | **Uaminifu na Maadili katika Biashara**<br>*(Business Ethics & Trust Building)* | Kozi hii inalenga kujenga misingi imara ya uaminifu na maadili katika uendeshaji wa biashara kwa maendeleo endelevu.<br>**Malengo na umahiri:**<br>• Kuelewa umuhimu wa maadili katika biashara.<br>• Kujenga uaminifu kwa wateja na wadau.<br>• Kuepuka vitendo vya udanganyifu na rushwa.<br>• Kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika biashara.<br>• Kusimamia sifa (reputation) ya biashara.<br>• Kutatua changamoto za kimaadili kazini. | • Wajasiriamali<br>• Wafanyabiashara<br>• Wasimamizi wa biashara | **120,000** |

| Na | Jina la Kozi | Malengo ya Kozi na Stadi Zitakazopatikana | Walengwa | Gharama (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| **13** | **Usimamizi wa Biashara Ndogo**<br>*(Small Business Management)* | Kozi hii inalenga kumwezesha mshiriki kuendesha biashara kwa ufanisi na kuongeza ushindani sokoni.<br>**Malengo na umahiri:**<br>• Kuelewa misingi ya usimamizi wa biashara ndogo.<br>• Kusimamia rasilimali (fedha, watu, vifaa).<br>• Kuandaa na kutekeleza mipango ya biashara.<br>• Kusimamia mauzo na masoko.<br>• Kufuatilia utendaji wa biashara (performance monitoring).<br>• Kufanya maamuzi sahihi ya kibiashara. | • Wamiliki wa biashara ndogo<br>• Wajasiriamali chipukizi<br>• Mameneja wa biashara | **150,000** |